



LOWELL PUBLIC SCHOOLS
Ofisi za Usimamizi wa Kati Henry J. Mroz
155 Merrimack Street
Lowell, MA 01852

Januari 25, 2021

Taarifa mpya kuhusu Hali ya Mafunzo ya Kuhudhuria Kibinafsi

Wapenzi Wanafunzi, Familia na Wafanyikazi wa Lowell Public Schools,

Huku tunapoendelea na mpango wa kurejelea upya wenye usalama kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi, Kamati ya Shule ilifanya mkutano wa pamoja na Bodi ya Afya ya Lowell siku ya Jumatatu, Januari 25, ili kujadili hali ya kisasa ya COVID-19 hapa Lowell.

Baada ya kuzingatia vipengele vyote – vikiwamo mienendo ya mwisho kabisa katika data ya kimtaa ya COVID-19 na hatari husika za afya na usalama kwa wanafunzi, wafanyikazi na jamii pana – Kamati ya Shule iliamua kuhairisha mwanzo wa tarehe zilizolengwa hapo awali kuanza kurejesha wanafunzi kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi kutoka Februari 1 hadi Februari 22.

Kwa hivyo, wanafunzi wote wa Lowell Public Schools wataendelea na mafunzo ya mbali hadi angalau wiki ya mapumziko ya Februari, huku tarehe zifuatazo zinazolengwa upya kwa wanafunzi kurejea kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi:

- Februar 22 – Wanafunzi katika programu za mafunzo maalum zilizotofauti zaidi na mafunzo ya kawaida ambao hapo awali walikuwa wanashiriki katika muundo wetu wa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi
- Machi 1 – Wanafunzi, ambao hawamo katika programu za mafunzo maalum zilizotofauti zaidi na mafunzo ya kawaida, lakini ambao walihudumiwa kibinafsi katika mwaka wa shule huu kama sehemu ya mpango wetu wa kufungua shule upya wa awali
- Aprili 1 – Upanuzi wa muundo wetu wa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi uwe na wanafunzi zaidi ya waliopangiwa kuhudhuria kibinafsi mwanzo wa mwaka huu wa shule

Ni muhimu kurejelea kwamba tarehe hizi si thabiti. Tutaendelea kurejelea data ya COVID-19 na kushauriana na Bodi la Afya. Pia tutahakikisha tunakupatia arifa zozote huku tukizingatia mpango wa mafunzo tukiendelea mbele.

Tunaendelea kuwa na shukrani kwa utendakazi wako wa pamoja na uwezo wenu wa kubadilika kirahisi huku tukijaribu kukabiliana na kutokuwa na hakika uliyoletwa na mgogoro huu wa afya usiyoshuhudiwa hapo awali.

Wako Mwaminifu,

Dr. Joel D. Boyd
Mkuu wa Mashule